

## **WARAKA WA PILI WA YOHANA KWA WATU WOTE**

<sup>1</sup> Mimi Mzee nakuandikia wewe Bimkubwa mteule, pamoja na watoto wako ninaowapenda kweli. Wala si mimi tu ninayewapenda, bali pia wote wanaoujua ule ukweli wanawapenda ninyi, <sup>2</sup> kwa sababu ukweli unakaa nasi milele. <sup>3</sup> Neema na huruma na amani zitokazo kwa Mungu Baba na kwa Yesu Kristo, Mwana wa Baba, zitakuwa pamoja nasi katika ukweli na upendo. <sup>4</sup> Nilifurahi sana kuona kwamba baadhi ya watoto wako wanaishi katika ukweli kama Baba alivy-otuamuru. <sup>5</sup> Basi, Bimkubwa, ninalo ombi moja kwako: tupendane. Ombi hili si amri mpya, bali ni amri ileile tuliyokuwa nayo tangu mwanzo. <sup>6</sup> Upendo maana yake ni kuishi kwa kuzitii amri zake Mungu. Amri niliyoisikia tangu mwanzo ndiyo hii: mnapaswa nyote kuishi katika upendo. <sup>7</sup> Wadanganyifu wengi wamezuka duniani, watu ambao hawakiri kwamba Yesu Kristo amekuja kwetu akawa binadamu. Mtu asemaye hivyo ni mdanganyifu na ni Adui wa Kristo. <sup>8</sup> Basi, jihad-harini ninyi wenyewe ili msije mkapoteza kile mlichokishugulikia, bali mpate tuzo lenu kamili. <sup>9</sup> Asiyezingatia na kudumu katika mafundisho ya Kristo, bali anayakiuka, hana Mungu. Lakini anayedumu katika mafundisho hayo anaye Baba na Mwana. <sup>10</sup> Basi, kama mtu akija kwenu bila kuwaleteeni mafundisho hayo, msimkaribishe

nyumbani kwenu, wala msimsalimu. <sup>11</sup> Maana anayemsalimu mtu huyo, anashirikiana naye katika matendo yake maovu. <sup>12</sup> Ninayo mengi ya kuwaambieni lakini sipendi kufanya hivyo kwa karatasi na wino; badala yake, natumaini kuwatembeleeni na kuzungumza nanyi ana kwa ana, ili furaha yetu ikamilike. <sup>13</sup> Watoto wa dada yako mteule wanakusalimu.

**Biblia Takatifu**  
**Portions of the New Testament in the Swahili**  
**Language of Kenya, Mozambique, Somalia, and**  
**Tanzania, translation by Dr. Johann Ludvig Krapf**  
**completed in 1850**

Public Domain

Language: Kiswahili (Swahili)

Dialect: Kimvita

Translation by: Dr. Johann Ludvig Krapf

2014-08-25

---

PDF generated using Haiola and XeLaTeX on 11 Nov 2022 from source files  
dated 9 Oct 2020

62071dc0-70e6-5b86-b569-c1b45e7771bd